Mwenye Ibada Bora

(The Worthy Worshiper)

na

Ellis P. Forsman

Mwenye Ibada Bora

(The Worthy Worshiper)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Mwenye Ibada Bora

Zaburi 15:

Daudi, Mtunzi, anaanza kwa kuuliza:

Zaburi 15:1, "*BWANA, ni nani atakayekaa katika hema yako? Ni nani atakayefanya maskani yake katika kilima chako kitakatifu?*"

Hii inaonyeshw akwamba kuna baadhi ya mahitaji ambayo yanatakiwa kutimizwa.

Katika mistari iliyobaki ya zaburi hii, anajibu swali hili.

Katika somo hili, tunapenda kuangalia ni nani anayeweza kufanikiwa kumwabudu Mungu.

Mtu aendaye kwa ukamilifu

Zaburi 15:2, "*Ni mtu aendaye kwa ukamilifu, na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake.*"

Kuna baadhi yaa maneno ya Kiibrania & Kiyunani ambayo yalitafsiriwa "nenda" na ambayo ina maana inayolandana:

- Tembea – ondoka.
- Tembea juu ya.
- Tembea katika msitari.
- Tembea ipasa.
- Tembea katika.
- Tembea njia.
- Tembea kwa haki, nidhamu njema.

Msitari huu unamanisha wale ambao hawainamii mapenzi ya Mungu wanapotembea.

Wale wanaotembea na Mungu.

- Nuhu. Mwan. 6:9, "*…Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu.*"
- Henoko. Mwan. 5:24, "*Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka maana Mungu alimtwaa.*"

- Ayubu. Ayubu 1:1, "*Palikuwa na mtu katika nchi ya Usi, jina lake alikuwa akiitwa Ayubu; mtu huyo alikuwa mkamilifu na mwelekevu, ni mmoja aliyemcha Mungu, na kuepukana na uovu.*"

"*Achwa*" – weka pembeni, epukwa.

Leo, wale wanaotembea katika nuru.

1 Yoh. 1:7, "*Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*"

Ni mtu aendaye kwa ukamilifu

Zaburi 15:2, "*Ni mtu aendaye kwa ukamilifu na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake,*"

Mwan. 7:1, "*BWANA akamwambia Nuhu, ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki.*"

Inawakilisha njia ya Mungu – amri zake.

Injili yake. Rum. 1:16-17, "*Kwa maana siionei haya Injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Yesu alitimiza haki ya Mungu alipobatizwa.

Mat. 3:15, "*Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali.*"

Asemaye kweli kwa moyo wake

Zaburi 15:2, "*Ni mtu aendaye kwa uaminifu, na kutenda haki. Asemaye kweli kwa moyo wake,*"

Kuna kanuni kuu mbili za kuishi:

Ukweli na uongo.

Mungu ni mwanzilishi wa ukweli. Heb. 6:18, "*Ili kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema uongo, tupate faraja iliyo imara sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yawekwayo mbele yetu.*"

Shetani ni mwanzilishi wa uongo. Yohana 8:44, "*Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakusimama katika kweli, kwa*

kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo asema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo na baba wa huo."

Tunawajibika kujifunza na kusema kweli.

Yoh. 8:32, "*Tena mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.*"

Yesu ndiye kweli. Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia, mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*"

Ni aina pekee ya ibada ambayo Mungu anaikubali.

Yoh. 4:24, "*Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"

Asiyesingizia kwa ulimi wake

Zaburi 15:3, "Asiyesingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, wala hakumsengenya jirani yake."

Ulimi lazima uongozwe kwa mambo mazuri.

Yakobo 3:3-18, "*Angalieni twatia lijamu katika vinywa vya farasi, ili wamtii, hivi twageuza mwili wao wote. Tena angalieni merikebu; ingawa ni kubwa kama nini, na kuchukuliwa na pepo kali, zageuzwa na usukani mdogo sana, kokote anakoazimia kwenda nahodha. Vivyo hivyo ulimi nao ni kiungo kidogo, nao hujivuna majivuno makuu. Angalieni jinsi moto mdogo uwashavyo msitu mkubwa sana. Nao ulimi ni moto ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi umewekwa katika viungo vyetu, nao ndio uutiao mwili wote unajisi, huuwasha moto mfulizo wa maumbile, nao huwashwa moto na jehanam. Maana kila aina ya wanyama na ya ndege, nay a vitambaavyo, na ya vitu vilivyomo baharini, vinafugika, navyo vimekwisha kufugwa na wanadamu. Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga; ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti. Kwa huo twamhimidi Mungu Baba yetu, na kwa huo twawalaani wanadamu walifanywa kwa mfano wa Mungu. Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana. Ndugu zangu haifai mambo hayo kuwa hivyo. Je! Chemchemi katika jicho moja hutoa maji matamu na maji machungu? Ndugu zangu, Je! Mtini waweza kuzaa zeituni, au mzabibu kuzaa tini? Kadhalika chemchemi haiwezi kutoa maji ya chumvi na maji matamu. N'nani aliye na hekima na ufahamu kwenu? Na aonyeshe kazi zake kwa mwenendo wake mzuri, katika upole na hekima. Lakini mkiwa na wivu wenye uchungu na ugomvi mioyoni mwenu, msijisifu, wala msiseme uongo juu ya kweli. Hekima hiyo siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya dunia, ya tabia ya kibinadamu na Shetani. Maana hapo palipo wivu na ugomvi ndipo palipo machafuko, na kila tendo baya. Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda*

mema, haina fitina, haina unafiki. Na tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani."

Mtu anayeabudu anawezaje kuulegeza ulimi wake na atarajie kukubaliwa na Mungu katika ibada?

Hili ni jambo moja wapo ambalo Paulo aliliogopa ambalo angelipata Korintho.

2 Kor. 12:20, "*Maana nachelea nisije nikawakuta si kama nitakavyo kuwakuta, nikaonekana kwenu si kama vile mtakavyo; nisije nikakuta labda fitina na wivu, na ghadhabu, na ugomvi, na masingizio, na manong'onezo, na majivuno, na ghasia;*"

Wala hakumtenda mwenziwe mabaya

Zaburi 15:3, "*Asiyesingizia kwa ulimi wake. Wala hakumtenda mwenziwe mabaya, wala hakumsengenya jirani yake.*"

Kama Mkristo, tunapaswa kuwajenga wenzetu, siyo kuwaangamiza.

Kuongea maovu yaw engine ni kuongeza mafuta kwenye moto.

Mit.26:20, "*Moto hufa kwa kukosa kuni; na bila mchongezi fitina hukoma.*"

Jirani mwema anatafuta njia ya kuwasaidia wengine.

Luka 10:29-37, "*Naye akitaka kudai haki, alimwuliza yesu, na jirani yangu ni nani? Yesu akajibu akasema, mtu mmoja alishuka toka Yerusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi; wakamvua nguo, wakamtia jeraha, wakaenda zao, wakimwachaa karibu na kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile; na alipomwona alipita kando. Na Mlawi vivyo hivyo, alipofika pale akamwona, akapita kando. Lakini Msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika hapo alipo; na alipomwona alimhurumia, akakaribia, akamfunga jeraha zake, akizitia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema mtunze, na chochote utakachogharimiwa zaidi, mimi nitakaporudi nitakulipa. Waonaje wewe katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi? Akasema ni huyo aliyemwonea huruma. Yesu akamwambia enenda zako, nawe ukafanye vivyo hivyo.*"

Uhusiano tulio nao na majirani zetu una maana katika ibada zetu.

Yeye anayeheshimu wamwogopao Mungu

Zaburi 15:4, "*Machoni pake mtu asiyefaa hudharauliwa, bali huwaheshimu wamchao BWANA ingawa ameapa kwa hasara yake, hayabadili maneno yake.*"

Mungu anataka watoto wake kuwaheshimu wale wanaomwogopa Mungu.

Mungu anaona uzuri katika wale wanaoishi maisha ya kiungu.

Zaburi 1:1-6, "*Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya BWANA ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando yaa vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa. Sivyo walivyo wasio haki; hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo. Kwa hiyo wasio haki hawata simama hukumuni, wala wakosaji katika kusanyiko la wenye haki. Kwa kuwa BWANA anaijua njia ya wenye haki, bali njia ya wasio haki itapotea.*"

Tunapaswa kuwaheshimu wengine wanaomfanyia Bwana kazi.

Hitimisho

Ni heshima kuu kuingia katika nyumba ya Mungu kufanya ibada.

Tunapaswa kujitahidi kutimiza mahitaji yake ya ibada.

Yohana 4:24, "*Mungu ni Roho, nao <u>wamwabuduo yeye</u> imewapasa kumwabudu <u>katika roho na kweli.</u>*"

Je wewe ni mwenye ibada bora?